

# UJUMUISHAJI WA FEDHA KIDIJITALI ILI KUFAULISHA **SOKO MOJA LA KIAFRIKA**

Afrika ipo katika hatua muhimu ya kukwamua watu milioni 30 kutoka katika umaskini kufikia mwaka 2035, kuimarisha mapato ya mamilioni zaidi,[1] na kuwasaidia wengine zaidi ya milioni 270[2] ambao ni wakazi wa maeneo ya mipakani kwa kuunda Soko Moja la Kiafrika.[3] Tunaweza kutumia nafasi hii kuhakikisha kwamba kila Mwafrika amewezeshwa kifedha na kiuchumi kufikia mwaka 2035. Hudumu za fedha za kidijitali, husussan malipo ya kidijitali, yamedhibitisha[4] uwezo wake wa kuyabadilisha maisha, jamii, na uchumi. Kuzifanya huduma hizi ziwajibike[5] na kupatikana kokote ndiyo changamoto ya hima, na nafasi iliyowekwa mbele yetu.

Malipo ya kidijitali yatakapotolewa kwa uwajibikaji, uwezo wa chumi za kiAfrika utafunguliwa.

Wakati ambapo ujumuishaji wa kweli wa kifedha kidijitali utakapofikiwa, yeyote anayeiita Afrika nyumbani atakuwa na nafasi ya kupaa na kufikia uwezo wake kamili, husussan wanawake na vijana, ambao ndio wengi barani, kwa takriban asilimia 60[6] ya idadi ya watu wa Afrika wenye umri wa chini ya miaka 25.

**Mkutano Mkuu wa Kiuchumi wa Duina (World Economic Forum) unahesabu kwamba asilimia 70[7] ya thamani mpya itakayotengenezwa duniani katika mwongo ujao, itawezeshwa kidijitali.** Umoja wa Afrika unatambua kwamba hii ni nafasi ya aina yake. Mwito huu wa kutenda kutoka kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, na Sekretarieti ya Eneo la Biashara Uhuru la Bara la Afrika (AfCFTA)[8] wanachukulia historia ya kujivunia ya Afrika ya uvumbuzi katika malipo ya kidijitali[9] kama msingi wake.

**Ujumuishaji wa Kifedha Kidijitali ni chombo chenye nguvu kilichothibitishwa.** Manufaa yake yenye ushawishi ni ya kimsingi na yenye faida nyingi. Una faida katika shughuli za kiuchumi[10] kwa kuongeza utendaji bora,[11] kupunguza gharama[12] na kuwezesha kushiriki kikamilifu kwa wanawake.[13] LUchumi jumuishi wa kidijitali utakuwa muhimu kwa mafanikio ya Sekretarieti ya Eneo la Biashara Uhuru la Bara la Afrika (AfCFTA). Malipo kidijitali ni muhimu katika kudijitisha biashara. Kufanikiwa kwa ujumuishaji wa fedha kidijitali kwa Waafrika wote kutaupa nguvu Umoja wa Afrika kutimiza ahadi[14] zake kwa wanawake na vijana katika mwongo ujao. Kushiriki kwa ujumla kwa wanawake na vijana kutahakikisha uchumi mbalimbali unafanyika katika viwango kamili, bila kutetereshwa na utengwaji. Uchumi jumuishi kidijitali unaupa kasi ufikiaji wetu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu,[15] na hasa Ajenda ya Afrika ya 2063.[16] Ujumuishaji wa uchumi kidijitali ni jambo la lazima katika kuyafikia yote mawili.

Katika mwaka wa 2021, ilikadiriwa kwamba asilimia 68, yaani, jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 36.6 zya biashara kwa njia ya simu za mkononi duniani, hufanyika Afrika.[17] Hii inaonyesha uwezo mkubwa uliopo katika huduma ya biashara ya kifedha. Hata hivyo, biashara hii inaweza kuingiza mfumo wa utengaji na kuongeza zaidi tofauti za kijamii kama utatekelezwa kwa kutowajibika. Umoja wa Afrika unatoa wito kuwe na mfumo wa ulipaji kidijitali wenye kuwajibika, uliosawazishwa, na bora kuliko malipo ya pesa taslim.

African Union

## Malengo yetu ya kuunda Soko Moja la Kidijitali la Afrika ili kuafikia Afrika tunayoitaka ni makubwa.

Safari ya Afrika kufikia Ujumuishaji wa Fedha Kidijitali[18] usiomwacha mwafrika yeyote nyuma una **mihimili mitano muhimu:**

**01** Uongozi wa serikali / **02** Sheria za wezeshi / **03** Utumiaji unaoaminika kwa wote / **04** Ushirikiano wa kikanda / **05** Usawa wa kifedha

**Mwito wa utekelezaji wa kila hatua unaonyesha jinsi malengo haya yanavyoweza kuafikiwa.**

### 01 / Uongozi wa serikali

Serikali ni kitovu katika kuongoza matumizi ya huduma za kifedha za kidijitali. Serikali ni lazima zielekeze jitihada za kujenga huduma zenye kutegemeka na kuwajibika na sizizomwacha yeyote nyuma.

**Mwito wa utendaji**

- Kufafanua ramani ya ujumuishaji wa huduma za kifedha za kidijitali, na kuwashawishi wadau wote wa kitaifa ili kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wake.
- Kufanya huduma zote na malipo ya serikali kuwa za kidijitali.
- Kuhimiza na kuunga mkono uvumbuzi.

### 02 / Sheria za uungaji mkono

Huduma za fedha za kidijitali hubadilika kila mara ili kuwahudumia watu vyema. Sheria ni lazima ziende na kasi hiyo.

**Mwito wa utendaji**

- Inahitaji utendaji-pamwe wa kitaifa na kikanda wa malipo ya kidijitali ili kuhakikisha kuna uwezo wa kuchangua na unafuu wa bei.
- Kuhakikisha ulindaji wa wateja[19] kupitia kwa mfumo uliolenga mtumiaji ili kujenga uaminifu. Sheria za Umoja wa Mataifa za Malipo ya Kidijitali yenye Kuwajibika[20] zinatoa mwongozo muhimu.
- Kuhakikisha kwamba masharti ya kitaifa yanaendana na makubaliano ya bara ili kumnufaisha kila Mwafrika.

### 03 / Utumiaji unaoaminika kwa wote

Wakati Watoa Huduma za Kifedha(FSPs) wanaposarifu huduma zao kwa kuwajibika, kwa kuzingatia mahitaji ya mtumiaji katika kina cha bidhaa, uaminifu unajengeka, na ukubalifu wa mtumiaji unafuata.

**Mwito wa utendaji**

- Kuhakikisha Watoa Huduma za Kifedha (FSPs) wanabuni bidhaa ambazo zinakidhi mahitaji ya watumiaji na wanapima kufaulu kwake kila wakati dhidi ya mahitaji hayo.
- Kuhakikisha wafanyabiashara wadogowadogo na wale wa kati wanaweza kupata huduma za kifedha kwa bei nafuu.
- Kuhakikisha Watoa Huduma za Kifedha (FSPs) wanatoa jawabu dhahiri, na fedha za wateja ziko salama.

### 04 / Ushirikiano wa kikanda

Malipo ya kidijitali yanaweza kupiku pesa taslim kama yatafanywa haraka, yakiwa salama, ya kutegemeka na ya kuaminika. Mashirika ya kibara na ya kikanda yana uwezo wa kufanikisha hili kwa pamoja.

**Mwito wa utendaji**

- Kushabikia wa Kiafrika ili kusukuma matokeo, kujenga uaminifu, na kutia kasi juhudi za kikanda.
- Kuhakikisha utendaji-pamwe wa mifumo ya malipo ili kurahisisha malipo kitaifa na kimipaka (taifa hadi taifa), kupitia kwa *Smart African Alliance*, na *Association of African Central Banks*. Kufikia utendaji-pamwe wa malipo kunahitaji viwango vinavyotumika sawa kama vile Mfumo Mmoja wa Kiafrika.[21]
- Kuwezesha ugavi wa maarifa na uzoefu kupitia mabadilishano kati ya jamii.

### 05 / Usawa wa kifedha

Kuhakikisha kila Mwafrika anashiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali bila kujali jinsia, umri au hadhi katika jamii. Wote wasiopata huduma na waliotengwa ni lazima wawezeshwe kwa huduma za kifedha za kidijitali wanazohitaji ili kuwawezesha kuishi maisha bora.

**Mwito wa utendaji**

- Serikali ichagize ujumuishaji wa wanawake, vijana na vikundi vilivyotengwa kama nafasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mpango Maalum na Mbinu Tendaji za Ujumuishaji wa Kifedha na Kiuchumi wa Wanawake[22] wa Umoja wa Afrika unaweza kuyaongoza Mataifa Wanachama.
- Serikali zitatathmini maendeleo ya kuelekea usawa wa kiuchumi[23] kupitia takwimu zilizochambuliwa kuonyesha jinsia na kutumia takwimu hizo kutekeleza sera muhimu kwa vitendo.
- Watoa Huduma za Kifedha wahusishe wanawake na vijana katika mchakato wote wa utengenezaji wa bidhaa ili kuhakikisha bidhaa mpya zinafaa kwa mahitaji yao.

Kila Afrika inapoangaliwa, mifano ya huduma za kifedha za kidijitali zenye ufanisi wa kubadilisha uchumi na jamii imejaa. Tunaweza kueneza mtazamo huo kwa maeneo na kwa watu ambao bado hawajatambua manufaa ya mpango huu muhimu. Afrika ni **kiongozi**[24] **katika maeneo muhimu**, hasa majukwaa ya kidijitali na mazingira yenye uungaji mkono kisheria ambayo yanajibu kwa haraka jinsi teknolojia inavyobadilika. Serikali, wasimamizi, na sekta-binafsi ni lazima wachukue fursa hii kujenga mazingira ya baadaye ambapo Waafrika wote watanufaika kutokana na faida za kidijitali, bila kuzingatia utaifa, umri, au nafasi ya mtu katika jamii. Hili sanasana ni muhimu katika kufikia usawa wa kiuchumi kwa wanawake na kuongeza kushiriki kwao katika uchumi.

Masomo kutoka kwa majukwaa na bidhaa za Afrika zinazoongoza duniani yanaweza kuchangiwa na kutekelezwa katika bara lote ili kuufanya ujumuishaji wa kifedha halisi kwa Waafrika bilioni 1.3.[25] Tuna kila kinachohitajika kuafikia ujumuishaji wa kifedha mara moja katika mwongo huu, ili kwamba, Soko Moja la Kiafrika tunalolijenga, liwe ni hilo ambalo vijana wa Afrika watajiona wenyewe wakiendelea na kufanikiwa kama tulivyolenga kwa Afrika tunayoitaka.

SCAN ME

Marejeleo ya mwisho

Kwa kushirikiana na: BETTER THAN CASH ALLIANCE, smart africa